

Je, ninahitaji kitambulisho ili kupata chanjo ya BILA MALIPO ya COVID-19?



Kila mtu anaweza kupata chanjo. SI LAZIMA uwe na bima ya afya, au uwe raia au mkazi wa Marekani. Huhitaji nambari ya ustawi wa jamii ili kupata chanjo, lakini watoa huduma wanaweza kukuuliza nambari hii ili waweze kuregeshewa gharama ya chanjo.

Ikiwa hukumbuki nambari yako ya ustawi wa jamii au hauna yoyote, unaweza kusema "hapana" wanapouliza. Hawatoi maelezo yako yoyote kwa idara ya uhamiaji au watekelezaji wa sheria.

Chanjo ni ya BILA MALIPO kwa kila mtu. Ikiwa una bima, watoa chanjo wanaweza kulipisha bima yako ada ya kutoa chanjo, lakini haupaswi kulipishwa chochote au kuombwa ulipe baadaye.

Lazima ulete kitu ambacho kinaonyesha jina lako (kama kitambulisho cha picha, bili ya matumizi, au barua iliyosainiwa kutoka kwa mtu anayethibitisha utambulisho wako).


Mifano ya aina zingine za kitambulisho unazoweza kutumia zilizo na jina lako:



Kitambulisho cha serikali kinachotolewa kwa wageni




Kitambulisho cha shule




I-94



Leseni ya udereva au pasipoti iliyoisha muda wake.




Kadi ya udereva ya nchi nyingine ambayo haitumiki kama kitambulisho.



Bili ya matumizi



Hati nyingine yoyote iliyo na jina lako



Kitambulisho cha makao